TAREKHE YA WANAVYUONI WA ZANZIBAR

SHEIKH SULEIMAN BIN MUHAMMAD AL-ALAWY (1900 AD – 1970 AD)

Muslim Academy

Ukutani

SHEIKH SULEIMAN BIN MUHAMMAD AL-ALAWY

Jina lake

Sheikh Suleiman bin Muhammad bin Suleiman bin Said Al-Alawy, ameitwa Al-Alawy kutokana na kabila lake kuitwa hivyo ambalo ni moja ya kabila mashhuri la Kiomani lilioko katika kijiji cha Yunqil nchini Omani.

Kuzaliwa na Kulelewa kwake

Sheikh Suleiman alizaliwa katika kijiji cha Mtetema Kaskazini "B" Unguja mwaka 1318 AH (1900 AD).

Babu yake Sheikh Suleiman ndiye aliehamia Unguja kutoka Oman.

Sheikh Suleiman alilelewa katika kijiji alichozaliwa huko Mtetema, na akasoma Quran kwa mwalimu Mwinyi Kombo.

Kusoma kwake na Mashekhe zake

Sheikh Suleiman alibahatika kuwa na Mashekhe wengi waliokuwepo Zanzibar, Misri, Makka, Madina na kwengineko. Pia alibahatika kusoma fani nyingi sana na kila fani alisoma vitabu vingi. Baadhi ya Mashekhe wake na vitabu alivyosoma kwao yamo katika Ijaza yake mashhuri.

Miongoni mwa Masheikh zake pamoja na aliyoyasoma:

1. **Sheikh Muhammad bin Khalfan (Haji Suwedi)**, alisoma kwake elimu za Kiarabu Nahw, Sarfa, Balagha, Aadabu, Usooli-Din, Fikhi, Tasawuf vitabu vya Imamu Ghazali na Mawlana Haddad.
2. **Sheikh Muhsin bin Ali Barwany**, Alisoma kwake Tafsiri ya Quran, Sahih Bukhari, Ihyaa Ulumi-Din, Fathul-Wahhaab, Iqnai

sherehe ya Abi Shujaa, Mantiq, Nahw. Pia alibahatika kuchaguliwa na Shekh Muhsin asomeshe pahala pake.

3. **Sheikh Abubakar bin Abdalla Bakathir**, alisoma kwake elimu ya Tafsiri, Hadithi na Mustalah wake, Ihyaa Ulumi-Din na Vitabu vya Aal-Baalawy. Nae alimpa idhini ya kusomesha katika Madrasa ya baba yake (Ukutani) fani za Balagha, Mustalah na Mantiq.
4. **Sheikh Ahmad Muhammad Mlomry**, alisoma kwake vitabu vya hadithi Mukhtasar Abi Jamra, Arbaina Nawawi, Shamail Muhammadiya, pia alisoma Madihi na Minhaji Taalibina kitabu kikubwa kusomeshwa cha Fiqhi ya Kishafii.
5. **Sheikh Abdalla bin Muhammad Bakathir**, amesoma kwake fani za Nahw, Balagha na kitabu cha Ihyaa Ulumi Din.
6. **Alhabib Omar bin Ahmad bin Sumeit**, amesoma kwake vitabu vya Tasawuf vikiwemo Ihyaa Ulumi-Din na vitabu vya Aal-Baalawy,Tajridi-Sarih (Mukhtasar ya Sahih Bukhari) na kampa ijaza ya vitabu vya Fikhi zaidi ya thalathini vikiwemo sherehe za Minhaaj, vitabu vya Sheikh Zakariya Al-Ansaari, Ibn Hajar Al-Haitamy, Shihaab Ramli, Al-Khatib Sharbiini. Pia alimpa ijaza ya kitabu Al-Adhkaar cha Imam Nawawi, na Sahih Bukhari.

Pamoja na kusoma kwa Mashekhe wengi wa Kisunni pia alisoma kwa baadhi ya Mashekhe wa Kiibadhi waliokuwepo Zanzibar wakati huo wakiwemo Sheikh Seif bin Nassor Al-Kharusi, Sheikh Nassor bin Salim Al-Rawahi na Sheikh Qaswar bin Humud Ar-Rashidy.

Madhehebu yake

Sheikh Suleiman alikuwa Sunni katika Aqida, akifuata Madhehebu ya Kishaafii katika Fiqhi, na alikuwa na Tariqa ya

Aal-Baalawy katika Tasawuf.

Kusomesha kwake

Sheikh Suleiman alikuwa na jitihada ya aina yake katika kusomesha, alikuwa kila wakati ana darasa popote alipo iwe mjini, shamba na hata anapotokezea kusafiri kwenda Dar-es-Salaam huweka darasa.

Miongoni mwa sehemu alizosomesha ni kama zifuatavyo:

1. **Shamba alikozaliwa na kukulia,** kabla ya kuhamia mjini, Sheikh Suleiman akisomesha shamba Kazole kwa nyakati tofauti, alisomesha fani mbalimbali na watu wengi walinufaika nae.
2. **Ukutani iliyokuwepo Mkunazini mjini Unguja,** kilikuwa ni kituo kikubwa cha elimu hapa Zanzibar kilichoanzishwa na Sheikh Abdalla Bakathir, walikuwepo Mashekhe mahiri wakisomesha na hata Sheikh Suleiman alipata kusoma hapo kwa Sheikh Abdalla na kwa Mashekhe wengine. Sheikh Suleiman aliteuliwa kudarasisha hapo tokea wakati wa mashekhe zake wakiwemo Sheikh Muhsin bin Ali Barwany na Sheikh Abubakar Bakathir na walipofariki wanafunzi wa Sheikh Abdalla Bakathir yeye ndie akashika makamu yao na kuendeleza kusomesha fani alizojaaliwa na Mola wake na kuimarisha Ukutani kielimu. Darasa za Ukutani zilikuwa zikianza asubuhi baada ya kumaliza nyiradi (wakati wa Ishraki) na kuendelea hadi nyakati za mchana.
3. **Msikiti Gofu uliopo Mkunazini mjini Unguja,** ni moja ya kitovu cha elimu mjini Zanzibar kwa wakati huo, Mashekhe wengi walisomesha hapo fani tofauti. Sheikh Suleiman nae alipohamia mjini Darasa zake zilikuwa Msikiti Gofu pia baada ya kupewa idhini ya kudarisisha. Darasa za Msikiti Gofu zilikuwapo asubuhi kwa baadhi ya siku, na darasa za kudumu zilikuwa baina

ya Magharibi na Isha. Pia alikuwa na darasa za nyakati tofauti hata zile za usiku wa manane. Sheikh Suleiman alishika darasa zote za Ukutani na Msikiti Gofu tokea mwaka 1377 AH (1957) mpaka kufariki kwake mwaka 1390 AH (1970).

4. **Maahad Islamiy (Muslim Academy) iliyokuwepo Forodhani mjini Unguja,** hiki kilikuwa ni chuo rasmi kilichofunguliwa na Serikali ya wakati huo na kilisheheni Wanavyuoni waliosomesha fani tofauti, nacho kilikuwa ni miongoni mwa vituo vikubwa vya elimu ya dini kwa wakati huo. Sheikh Suleiman alikuwa akisomesha Maahad Islamiy fani mbalimbali na kushirikiana na Mashekhe wa hapo waliokuwa wakitoka nchi mbalimbali zikiwemo wenyeji wa Zanzibar, Lamu Kenya, Hadhramout, Misri n.k.

Sheikh Suleiman alivisomesha takribani vitabu vyote alivyosoma kwa Mashekhe zake alivyovitaja katika Ijaza yake na vengine asivyovitaja mfano Fathul-Muiin, Shifaa ya Qadhi Iyadh na venginevyo.

Mambo Aliyotuwachia

Sheikh Suleiman ametuachia hazina kubwa ya andiko lake la IJAZA. Aliwapa Ijaza hio mabwana watatu nao ni:

1. Alhabib Abdalla bin Ahmad bin Abdalla Al-Haddaar.
2. Sayyid Hadi bin Ahmad bin Abdalla Al-Haddaar.
3. Sayyid Omar bin Abdalla bin Sheikh (Mwenye Baraka).

Ijaza hio ameiandika kwa ufundi mkubwa na inatowa taswira ya elimu yake aliyoipata kwa kwa baadhi ya Masheikh zake wa Unguja na wale waliotembelea Unguja, Masheikh wa Dar-es-Salaam, pamoja na aliowatembelea Makka, Madina na Misri.

Aidha anaelezea katika Ijaza hiyo namna alivyotangulizwa kudarisisha, nyiradi alizopewa ijaza na faida nyingi nyenginezo.

Ijaza hiyo ni muhimu sana kwa kujuwa silsila ya elimu ya Mashekhe wa Zanzibar na Afrika Mashariki kwa ujumla na ambayo Alhabib Omar bin Ahmad bin Sumeit aliisifu sana.

Pia Sheikh Suleiman alipokuwa Dar-es-Salaam alimtungia mwanafunzi wake Sheikh Muhammed Kisawaga kitabu kidogo cha Nahw ambacho hakijachapishwa na kwa wale waliosoma Muslim Academy wamesimulia kuwa alikuwa akiandika ubaoni kile anachokisomesha na hakuwa akitumia kitabu kimoja kwa baadhi ya fani.

Wanafunzi Wake

Sheikh Suleiman alikuwa na wanafunzi wengi sana, miongoni mwao walidarisisha katika uhai wake darasa za Msikiti Gofu na wengine walisomesha sehemu zingine visiwani Unguja na nje ya mipaka yake. Baadhi ya wanafunzi wake ni:

1. Sayyid Ahmad Yasin.
2. Sayyid Omar bin Abdalla (Mwenye Baraka).
3. Sheikh Muhammad Salim Makka Annofliy.
4. Sheikh Shaabani bin Zahor.
5. Sheikh Abdalla Ayoub wa TAMTA, Tanga.
6. Sayyid Muhammad Adnaan Aideed.
7. Sayyid Abubakar (Shibli) Omar Qullatein.
8. Sayyid Ali Omar Qullatein.
9. Sayyid AbdulQadir bin AbdulRahman Al-Juneyd.
10. Sheikh Harith bin Khelef Al-Ghaithy, aliyekuwa Mufti Mkuu wa Zanzibar.
11. Sheikh Muhammad Mansoor.

12. Ustadh Muhammad bin Shariff Said Albiidh.
13. Sheikh Khamis bin Said wa Mtoni Dar-es-Salaam.
14. Sheikh Saleh Omar Kaabi, Mufti Mkuu wa Zanzibar.
15. Sheikh Machano bin Khamis.

Na wengine wengi ambao wametawanyika kila sehemu ya Afrika Mashariki, tuliowataja ni baadhi tu kuhofia kurefusha.

Kazi Alizofanya

Kuna wakati Sheikh Suleiman alihamia Dar-es-Salaam na kufanya shughuli za usafirishaji (Tansport).

Sheikh Suleiman pia alikuwa Tabibu wa maradhi ya kienyeji na alikuwa hachagui nani wa kumtibu, akitibu watu wa kabila zote na dini tofauti.

Kizazi Chake

Sheikh Suleiman alikuwa na watoto wawili wa kiume na wawili wa kike. Watoto wa kiume ni Dr. Zamil aliyefariki Dar-es-Salaam na Sheikh Muhammad aliefariki nchini Emarati. Ama binti zake wawii mmoja amewacha kizazi na mmoja hakuwa na kizazi.

Sheikh Suleiman alikuwa na ndugu yake aliekuwa akiitwa Sheikh Zamil bin Muhammad Al-Alawy ambae pia aliruzukiwa kizazi.

Kutaka Kuhama

Baada ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliofanyika mwaka 1964, Sheikh Suleimani alielekea Kampala nchini Uganda kwa Sheikh wake Alhabib Ahmad Mashuur Al-Haddad na kumtaka shauri la kuhama Unguja. Alhabib Ahmad akampatia kazi ya kusomesha

katika Chuo cha Kiislamu na Sheikh Suleimani akawafiki kupatiwa nafasi hio. Ilipofika siku ya kutiliana mkataba, Alhabib Ahmad Mashuur akamwambia Sheikh Suleiman kuwa Alhabib Omar bin Ahmad bin Sumeit anamuamrisha arudi Unguja na kuwa naibu wake huko Unguja. Sheikh Suleiman bila ya kubisha akauitikia ujumbe aliopewa na akarudi kuishi Unguja mpaka kufariki kwake.

Kufariki Kwake

Sheikh Suleiman alifunga macho mchana wa siku ya Ijumamosi, mwezi 26 Muharram 1390 AH (4 April 1970). Alisaliwa Msikiti Gofu na Sala ya maiti iliongozwa na mwanafunzi wake Sayyid AbduQadir bin AbdulRahman Al-Juneyd Jamali-Layl.

Kifo chake kilikuwa msiba mkubwa kwa watu wa Zanzibar, alizikwa Shambani kwake Nyanjale, Unguja.

Hizi ni miongoni mwa khabari za Sheikh Suleiman Al-Alawy, tumezitaja kwa ufupi kuepuka kumchosha msomaji.

Rejea:

1. *Ijaza ya Sheikh Suleiman aliowapa Mashekhe watatu.*
2. *Kitabu cha Syd. AbdulKadir bin AbdulRahman Al-Juneyd "Uqudul-Jaahizah".*
3. *Kitabu "Baadhi ya Wanavyuoni wa Mashariki ya Afrika" cha Sheikh Abdalla S. Farsy.*

Maahad Juneyd Islamiy
Kitengo cha Bahthi na Utafiti
+255 777 878 047 – Zanzibar